

# MKRISTO AKITAZAMA UWAKILI WAKE



# MKRISTO AKITAZAMA UWAKILI WAKE

# YALIYOMO

UTANGULIZI.......................... (i)

WEWE NI NANI MBELE YA MUNGU.......... 1

WEWE NI WAKILI WA NAFSI YAKO YOTE.... 8

WEWE NI MTOAJI MBELE YA MUNGU........ 13

WEWE NA SEHEMU YA KUMI............... 19

TARATIBU ZINAZOHUSIKA NA MATOLEO
YAKO................................. 24

MWISHO............................... 30

Published and printed by
Baptist Publications House
Box 30370, Likoni Rd., Nairobi

B. Vifungu Vya Kukaza -

1. Waefeso 6:5-7
2. I Wakorintho 4:2

# MWISHO

Sasa msomaji, umejifunza yale yaliyomo kitabuni humu. Lakini swali linalobaki ni kubwa zaidi. Swali si, "Umemaliza Masomo?" tu. Swali si, "Unafahamu mafundisho?" tu. Swali si, "Unakubali ya kuwa mafundisho haya ni kweli na vema?" tu; Swali ni, "Utajitoa kuyafuata mambo hayo ya uwakili wa Kikristo kwa nguvu katika maisha yako yote?"

Ikiwa wakubali ya kwamba wajitoa kuwa wakili anayestahili, sasa hivi kaa kimya mahali ulipo umwombe Mungu kwa bidii ukimwahidi kufuata kusudi lake katika maisha yako kwa njia ya UWAKILI WA MAISHA YAKO YOTE.

"Hapo tena inayohitajiwa katika mawakili,ndiyo mtu aonekana kuwa mwaminifu." I Wakorintho 4:2

A. Maswali Ya Kuzungumzwa -

1. Unaweza kuongeza matoleo yako kwa njia gani?

2. Je! Katika kazi yako kuna vitu gani vinavyoweza kuwekwa kando kabla hujahesabu matoleo yako?

3. Kanisa lako lina mahitaji gani katika matumizi ya pesa?

4. Kanisa lako linafuata mpango gani katika kuhesabu, kutunza, na kutoa ripoti juu ya pesa?



# UTANGULIZI

MKRISTO AKITAZAMA UWAKILI WAKE kimeandikwa kwa kusudi la kuwasaidia Wakristo kukua.

Kitabu hiki kilitayarishwa mara ya kwanza mwaka wa 1968. Kilitumika katika Jitihada ya Uwakili katika makanisa ya Kibatisti. Viongozi walituomba kupiga chapa tena kitabu hiki. Kitabu hiki kinapigwa chapa kusaidia Wakristo wote kuendelea na uwakili wao.

Kimeandikwa pia ili wachungaji wa makanisa na viongozi wengine mara kwa mara wataweza kuwafundisha washiriki wao juu ya uwakili kwa kukitumia kitabu hiki na masomo yaliyomo.

Pamoja na hayo, kimeandikwa ili Mkristo ye yote anayependa kumtumikia Mungu zaidi ataweza kukisoma na kuelewa wajibu wake kama Wakili wa Mwenyezi Mungu.

Dr. Davis Saunders aliyeandika kitabu hiki amekaa Afrika tangu mwaka wa 1953. Sasa Dr. Saunders ni kiongozi mkuu wa Chama cha Umisheni cha kanisa lake.

4. Mahitaji mengine kama msaada kwa wagonjwa fulani au maskini fulani kutumiwa kwa haja halisi ikitokea mara kwa mara. Matoleo kwa Jumuiya, kwa kusanyiko, na kwa jitihada zinazofanywa kwa kiasi chake. Hata pengine kufanya kazi ya umisheni kama kuanzisha kituo cha kuhubiri kwa mali palipo karibu na kanisa lako, au katika ushirika pamoja na makanisa mengine.

e) Hatua ya tano ni kupanga njia ya kusaidia watu kupima matoleo yao. Mpango huu unaweza kuwa na mambo yake ya asili pia kama yote yanayowekwa hapa.

1. Mpango usifanywe kama kodi au kama sharti juu ya mshiriki.

2. Mpango usiwe kwa tendo fulani kama ubatizo, chakula cha Bwana, mazishi, ndoa. n.k.

3. Mpango usiwe wa kumwaibisha anayekosa kutoa na kumsifu Bwana mbele ya watu watoao.

4. Mpango uwe msaada kwa mtu ajue wajibu wake kama wakili wa Mungu na mshirika wa kanisa.

5. Mpango uwe msaada kwa mtu kukumbuka kutoa kwa taratibu. Kila wakati na kwa kiasi kinachostahili uwakili wake.

6. Mpango uwe na njia ya kuonyesha uwakili wa pesa unafuatana na uwakili wa karama nyingine za Mungu, kwa uhai wetu, na Injili yetu.

wanaoacha hazina yao katika nyumba kwenye sanduku au mkebe tu, kwa sababu mara kwa mara pesa hizi zitaibiwa au kutumiwa na wale wasio na madaraka.

d) Hatua ya nne ni kupanga juu ya mahitaji ya kanisa katika mapokeo yake kwa mwaka mzima, na kulinganisha mapato na mahitaji yale. Hapo washiriki wote wanaweza kujua hali ya kanisa katika mambo ya fedha. Kila kanisa linaweza kupima kwa kufikiria jinsi inavyoendelea kwa kawaida. Mahitaji yao yatakuwa kama mambo yafuatayo:

1. Mahitaji ya nyumba ya kanisa. Pengine kujenga. Pengine kutengeneza. Pengine kuongeza. Pengine kupaka rangi (hata mahitaji ya maji na stima, mjini) n.k.

2. Mahitaji ya vitabu vya kanisa. Vitabu vya Masomo ya Shule ya Jumapili kwa wazima, watoto na waalimu. Vitabu vya nyimbo kwa kanisa, ili watu waweze kuimba vizuri, vitabu vya Ushirika Wa Wanawake Waenezao Injili ili wawe na mikutano mizuri. Vitabu vya "Maisha Yako Na Kanisa Lako" ili wanaojitoa wataweza kupewa kimoja kujua imani yao n.k.

3. Mahitaji ya mchungaji. Yule anayeshughulika kila saa na kazi ya kanisa, mapato yake yote kama mshahara wake. Yule anayefanya kwa sehemu ya wakati wake, kiasi kile kilichokubaliwa. Msaada ule wa nauli kwa mikutano ya jumuiya au kusanyiko, n.k.





# WEWE NI NANI MBELE ZA MUNGU?

## 1. U Mali yake Mwenyezi Mungu.

Daudi, Mfalme wa Israeli aliposema katika Zaburi 24:1, "Nchi na vyote viijazavyo ni mali ya Bwana, dunia na wote wakaao ndani yake," alieleza MSINGI WA MAISHA YOTE ya kila mwanadamu. Ukitupa macho yako kwa kuangalia dunia ambamo unaishi, kila kitu ambacho unakiona kimeumbwa na Mwenyezi Mungu; kila ndege, kila mnyama, kila mti, kila ua. Tena, ukitembea barabarani na kuwaangalia wote wanaokupita njiani, wote wameumbwa na Mwenyezi Mungu; kila mwanamume, kila mwanamke, kila mzee, kila kijana, kila mtoto. Ukijiangalia hali ulipo sasa; ukiwa wapi, ukiwa na hali gani, fahamu ya kuwa umeumbwa na Mwenyezi Mungu.

Fikiri, kila jioni ukilala usingizi kwako, usalama wako uko katika mikono ya Mwenyezi Mungu. Vile vile, kila asubuhi uamkapo na kupumua pumzi yako, kwa kuingia katika siku mpya ya kazi yako, ni Mwenyezi Mungu ndiye anayekuruhusu pumzi ile na siku ile.

Inakupasa kutambua jinsi unavyomtegemea Mungu kwa maisha yako yote. Kila tendo unalolitenda, kila neno unalolisema, na kila wazo unalolifikiria, litafanywa kwa kukumbuka kuwa pasipo nguvu ya Mwenyezi Mungu, Mwumbaji wako, uhai wako utakwisha.

Je! jembe linakwenda shambani na kulima bila mlimaji? Kalamu inaandika barua bila mkono wa mwandishi? Gari linakwenda safari yake dreva asipoliendesha mwenyewe? Vivyo hivyo unamtumainia Mungu kwa mambo yako yote. ANA AMRI YOTE JUU YAKO. Warumi 11:36 inasema, "Kwa kuwa vitu vyote vyatoka kwake, viko kwa uweza wake, tena vinarejea kwake."

2. Vyote Ulivyo Navyo Vyatoka Kwa Mungu.

Katika Yakobo 1:17, "Kila kutoa kuliko kwema,na kila kitolewacho kilicho kamili, hutoka juu, hushuka kwa Baba..." Hapa Biblia inataja jambo muhimu kwa kila Mkristo. Unahitaji kutambua ulivyo navyo hutoka wapi.

Wengi wetu ni walimaji, na hawa huelewa lazima ya jua, mvua na mavuno mazuri ikiwa watapata riziki za kutosha. Katika kitabu cha Matendo 14:17, twasoma, "Lakini hakujiacha pasipo ushuhuda, kwa kuwa alitenda mema,akiwapeni mvua kutoka mbinguni, na nyakati za mavuno, akiwashibisha mioyo yenu chakula na furaha."

Mara nyingi tunaona watu wenye mahitaji mengi kuliko sisi. Wale wanaokosa chakula au nguo au nyumba, au furaha yo yote. Na sisi tunayo ile ya kutufurahisha. Hatukai uchi, hatufi kwa njaa, tuna malazi yetu. Je! Mungu ndiye anayetuwezesha vitu hivi? Mara nyingi tunawaona wale wasiojiweza, wagonjwa, vipofu, viwete, na kadhalika. Ingawa mara kwa mara twapata maradhi, bado tuna uwezo wa kutosha. Mara nyingine wanazimika roho ghafula pengine



Kwanza jua ya kuwa wewe, kama mshiriki wa kanisa lako, unahusika na njia za kuweka na kutumia pesa zinazopatikana katika ushirika ule.

Kwa vile tunajaribu kutoa pesa kwa njia inayostahili kazi ya Bwana, tunahitaji kutunza na kutumia pesa zile pia kwa njia nzuri inayostahili kazi ya Bwana.

a) Hatua ya kwanza ni kuweka mapato ya kanisa kwa njia zinazofaa. Kanisa liwe na kitabu maalum ya pesa ya kanisa ambamo kila kupokea na kila kutoa kumeandikwa. Zaidi ya mtu mmoja wahesabu pesa kila mara na waandike sahihi zao kando ya tarehe ile na kiasi kile. Tena, kila kutoa kuandikwe na sahihi ya yule anayetoa, na kupatia cheti au stakabadhi kutoka wale wanaopokea pesa zile.

b) Hatua ya pili ni kuwa na sharti kwa waweka hazina kutoa ripoti inayofahamika katika mkutano wa shughuli za kanisa kila mara ikiwa ni mwezi mmoja, miezi mitatu - minne, au mwaka mzima. Wenye kazi hii wataeleza mapokeo kwa hatua yake, malipo kwa kila hatua, na mabaki kwenye hazina ya kanisa.

c) Hatua ya tatu ni kupanga njia ya kuweka pesa za kanisa zisiibiwe au kupotea. Wale wa makanisa ya mjini hawana shida kwa sababu wanaweza kuweka sehemu iliyo akiba au isiyohitajika katika Banki au Posta. Hata wale wanaoishi mbali wataweza kutuma pesa hizi mjini na mshiriki mwema akisafiri kwa shughuli zake. Makanisa mengine yanaomba wamisheni wao kuwasaidia kuweka pesa. Hatari iko kwa wale

yote. Unaweza kuuza sehemu ile mwenyewe sokoni na kuleta pesa zile zote kanisani. Au unaweza kuleta sehemu ile ya mavuno kanisani na viongozi wa kanisa wataweza kuuza kanisani. Au unaweza kukusanya matoleo ya mavuno ya wengi na kuyapeleka kuuza sokoni kwa ajili ya kanisa.

b) Njia nyingine ni kugawanya sehemu ya shamba lako na kuiweka kama sehemu ya Bwana na yote yaliyotoka humo itakuwa ya kanisa ukiuza na kuleta pesa kanisani au kuleta mavuno yote kanisani kuuzwa na viongozi.

c) Njia ya tatu ni kujitoa kufanya kazi kwa siku fulani au saa fulani na mapato ya siku na saa hizi yawe ya Bwana yakiwa pesa au mavuno.

d) Njia nyingine ni, kama kundi, kuligawia kanisa shamba lake kutoka kwa mashamba ya washiriki wote, na kanisa lisimamie kazi ya shamba lile, watu wakijitoa kulima kwa kundi au kuandika mtu kwa kazi ile. Mapato yote yakiwa ya kanisa.

Kwa jumla inaonekana ya kuwa njia ya kwanza ni bora kwa sababu kipimo ni kwa kiasi cha kufanikiwa au kubarikiwa kwa kila mtu binafsi katika riziki zote.

Tena tusisahau kuleta wanyama, kuku, mayai, na kadhalika kwa Mungu kama matoleo yetu.

2. Njia Za Kutumia Matoleo Yako Katika Kazi Ya Bwana.



pasipo kuonekana kama wagonjwa, wakipata ajali njiani, au jambo jingine. Je! na sisi, bado tuko katika hali ya kuweza kufanya kazi yetu au kufurahishwa na riziki zetu?

Kwa kweli, baraka zetu zote za maisha haya, nguvu tuliyo nayo, MAMBO HAYA YOTE HUTOKA KWA MWENYEZI MUNGU.

3. Wokovu Wako Hutoka Kwa Mungu.

Wewe kama Mkristo una kitu gani kinachokufaa kuliko mambo yote ama vitu vyote? Ikiwa wafikiri juu ya siku zote na mwenendo wa miaka utasema, 'Bila shaka uzima wangu.' Kwa sababu bila uzima vyote vingine havikufai. Lakini ukifikiri zaidi utaongeza maneno yale kuwa, 'Bila shaka uzima wangu wa MILELE na WOKOVU WANGU.'

Je! uzima wako wa milele na wokovu wako unatoka wapi? Katika I Wakorintho 6:19-20 Neno la Mungu lasema, 'Au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu? Wala ninyi si mali yenu wenyewe; maana mlinunuliwa kwa thamani.' Mungu aliyekuumba alizidi kuleta nguvu yake kwako katika kukufikiria. Kwa vile anajua nguvu ya dhambi na ya Shetani, ametayarisha njia ya kushinda dhambi na Shetani. Kwa sababu anaelewa ya kwamba mshahara wa dhambi ni mauti, ametufungulia mlango wa kutoroka malipo yale; yaani, wokovu wake. Kwa njia ya kumtuma Mwana wake, mpendwa wake, ili afe msalabani kwa ajili yako. Umepewa nafasi ya kuokoka na kuwa na uzima wa milele.

Je! pasipo Mungu na wokovu wake, ungeweza kutumaini nini baada ya maisha haya, yakiwa mafupi au marefu? Si ndiyo kuishi kwa roho yako au zaidi kuangamia? Wasiomjua Mungu na Yesu hawana la kufanya ila kuogopa kifo. Lakini Mkristo anajua mwenendo wake wa milele.

### 4. Kila Mtu Atatoa Habari Zake Mwenyewe Mbele ya Mungu.

Ingawa tumekwisha tambua ya kuwa uzima wa milele ni tumaini la kila Mkristo, tusisahau jambo moja kubwa. Kila mtu ataacha maisha ya dunia na mwili wake wakati wa kifo chake. Wengine huishi kwa muda mrefu, wengine hawakawii katika ulimwengu huu. Na wakati ule wa kifo, itakuwaje?

Mtume Paulo, akiongozwa na Roho Mtakatifu alisema katika Warumi 14:12, "Basi ni hivyo, kila mtu miongoni mwetu atatoa habari zake mwenyewe mbele za Mungu." Katika kifungu hiki waweza kujifunza mambo mawili.

Kwanza, hatua hii itachukuliwa na kila mtu, akiwa Mkristo au la. Unajua hakika ya kuwa siku moja utasimama hukumuni. Mambo yako yote yatajulikana wazi. Yale uliyoyatenda katika giza au kwa siri; matendo yako mema na matendo mabaya; matendo ya kujenga ufalme wa Mungu au kuubomoa; matendo yako yaliyosaidia na yale yaliyoumiza. Kila tendo, kubwa kwa dogo, litawekwa wazi katika wakati ule wa hukumu.

Pili, hukumu hii itakuwa mbele ya



navyo na wewe hutakuwa na aibu mbele ya mabwana wako wala Mungu Bwana wako wa kweli.

Mtu anayepokea riziki yake kwa biashara atahitaji kuwa mfanya kazi bora akijaribu kupima matoleo yake kwa Bwana katika njia hii, kwa sababu atapata kujua faida yake kwa jumla ni ngapi. Ikiwa anataka kuongeza matoleo yake atahitaji kutumia busara na bidii na njia zinazofaa katika biashara, akikaza mambo ya haki pamoja na kazi yake.

Mtu anayelima atahitaji kukumbuka ya kuwa mapato yake si pesa zinazopatikana kwa kuuza sehemu ya mavuno inayobaki baada ya kuweka akiba ya kutosha chakula cha jamaa. Mapato yake ni yote yanayobaki akiweka mbegu za kupanda na mshahara wa wasaidizi wake wasio wa jamaa yake, pamoja na matoleo kwa mbolea, dawa, na vyombo vyake.

Mkulima ataweza kuongeza mapato yake kwa bidii na busara yake ya kazi. Ataweza kutafuta njia zinazofaa zaidi katika ulimaji, kutafuta nafaka inayositawi vizuri zaidi, au mavuno yenye thamani kuu zaidi. Pia anaweza kuongeza sehemu ile anayolima kwa kutafuta njia za kuongeza shamba lake.

Vile vile ataweza kutafuta njia bora kupima sehemu ile ya matoleo kwa Mungu. Watu wengine wanatumia njia nyingine. Njia mbalimbali zitaelezwa sasa.

a) Njia moja ni kuleta sehemu ile ambayo umeamua kutoa kutoka mavuno yako

*SURA YA TANO*

## TARATIBU ZINAZOHUSIKA NA MATOLEO YAKO

### 1. Njia Unayoweza Kuhesabu na Kuongeza Kutoa Kwako.

Inakupasa kwanza kukaa na kutafuta mapenzi ya Mwenyezi Mungu katika kutoa kwako. Kabla hujaamua, rudi kwa ufupi kukaza mafundisho ya Biblia juu ya hali na mali yako kama yanavyoelezwa katika milango minne iliokwisha somwa. Mungu anakuongoza kufanya nini? Kutoa kwa hiari, furaha, ukarimu, na taratibu, sehemu ya Kumi? Kutoa kwa kiasi fulani kila juma au kila mwezi? Kusema haidhuru nitoe nini?

Mtu anayekaa mjini anayepokea mshahara wa pesa hana shida kujua jinsi ya kupima sehemu ya kumi wala utaratibu wa kutoa. Shida yake ni kujua njia yake ya kuongeza mapato yake ili aongeze matoleo yake. Hana la kufanya, ila kwa bidii yake na uaminifu wake kuonyesha jinsi anavyofanya kazi vizuri na kwa hiyo kupandishwa cheo au mshahara. Pengine mkazo wa Paulo katika Waefeso 6:5-7, juu ya watumwa, itakusaidia kama mfanya kazi ya mshahara. Inasema, "Watiini wao walio bwana zenu kwa jinsi ya mwili, kwa hofu na kutetemeka, kwa unyofu wa moyo, kana kwamba ni kumtii Kristo; wala si kwa utumwa wa macho tu kama wajipendekezao kwa wanadamu; bali kama watumwa wa Kristo, mkitenda yampendezayo Mungu kwa moyo; kwa nia njema kama kumtumikia Bwana wala si mwanadamu." Kwa hivyo bwana zenu watafurahi kwa vile unafanya vizuri iwezeka-



nani? Mwenyezi Mungu mwenyewe ni yule tutasimama mbele zake. Waweza kujua hukumu hii si mbele ya mama wala baba, si mbele ya ndugu wala dada, si mbele ya mchungaji wako wala mmisheni wako, hata si mbele ya hakimu wa serikali yako. Ni mbele ya yule ambaye U mali yake; yule ambaye vitu vyako vyote vyatoka kwake; yule ambaye alitoa wokovu wako na uzima wa milele.

Kwa sababu hizi, ana amri juu yako. Kumcha Mungu, kumwabudu, kumtumikia na kumpenda, wahitaji kuwa mtiifu wa mapenzi yake. Anapenda uwe mtu wa namna gani?

### 5. Kila Mkristo Anahitaji Awe Wakili Mwaminifu.

Kwa sababu ya mafundisho mengi, kazi ya Mkristo, hata hali yake, ni kuwa wakili mwaminifu. Kwa mfano katika I Wakorintho 4:1-2, imeandikwa, "Mtu na atuhesabu hivi, kuwa tu watumishi wa Kristo, na mawakili wa siri za Mungu. Hapo tena inayohitajiwa katika mawakili,ndiyo mtu aonekane kuwa mwaminifu." Na tena katika I Petro 4:10, "Kila mmoja kwa kadiri alivyopokea karama, itumieni kwa kuhudumiana; kama mawakili wema wa neema mbalimbali za Mungu."

Biblia imekaza ya kuwa kila mtu anapewa kwa matumizi ya uwakili wake katika kila kitu kutoka uzima wa milele na uhai wake mpaka afya, nguvu, uwezo, mapato na riziki zake. Hakuna sehemu yo yote ambayo twaweza kuweka kando na kusema, "Mungu hana uwezo juu ya jambo hili au kitu hiki." Kumbuka yule tajiri katika

maelezo ya Yesu ya Luka 12:20-21, Mungu aliposema, "Mpumbavu wewe, usiku huu wa leo wanataka roho yako!"

Mtu akisahau au akikataa Neno hili hana uwezo wa kujiepusha na ukweli huu. Na Mkristo akiona ya kuwa haki yake Mungu katika mambo hayo yote haina uhusiano naye, na wokovu wake. Pia, anajitenganisha na ushirika wake na Mwenyezi Mungu pamoja na baraka nyingi zinazotoka kwa Mungu.

Je! Watambua ya kwamba U Mali Yake Mungu? Je! wakubali Vyote ulivyo navyo vyatoka kwa Mungu? Je! Watambua kuwa Wokovu wako unapewa na Mungu? Je! Wafahamu jinsi utakavyosimama binafsi mbele ya hukumu ya Mungu siku ile? Ikiwa wasema, "Ndiyo" kwa maswali hayo manne, utaelewa sababu unahitaji kuwa wakili mwaminifu katika maisha yako yote.

A. Mambo ya Kuzungumzwa -

1. Una vitu gani maishani vinavyoletwa na msaada wa Mungu?

2. Unaweza kufanya jambo gani bila uwezo wa Mungu?

3. Unaweza kufanya nini kujiepusha na hukumu ya Mungu?

4. Waweza kuonyesha shukrani kwa baraka za Mungu kwa njia gani?



Je! Waweza kufikiria mambo haya mwenyewe? Watoa sehemu ya kumi kwa kanisa lako? Je! Wapima sehemu yako ya kumi kwa moyo gani?

A. Maswali ya Kuzungumzwa -

1. Mkristo analazimishwa kufuata sheria za Agano la Kale?

2. Kanisa linahitaji kutafuta njia nyingine za kupata pesa yake kuliko zaka au sadaka?

3. Njia ngapi zilizotajwa kufikiria uamuzi juu ya zaka zinatumiwa katika kanisa lako?

4. Jinsi gani unaweza kupima mapato yako katika kujua sehemu ya kumi ni ngapi?

B. Vifungu Vya Kukaza -

1. Luka 12:48
2. Malaki 3:8-12
3. Luka 11:42
4. Luka 18:12
5. Marko 10:17-22
6. Mathayo 6:33

4. Asili Ya Kupima Zaka Zako.

Pengine utasema kuwa utatoa sehemu ya kumi au zaka lakini hujui jinsi ya kugawanya, au kupima. Kuna mambo matano katika asili ya kujua ni kiasi gani.

a) Kumbuka ya kwamba zaka si kodi kuhesabika chini iwezekanavyo bila kuvunja sheria. Ukipima kodi yako, hakika, wapima kwa njia ya upungufu wa malipo. Si hivyo kwa matoleo kwa Mungu. Ni hiari na waweza kutokutoa mwenyewe.

b) Hakikisha mshahara wako wote au faida yako yote ya kila wakati. Mfanya biashara atahesabu faida na sio mapokeo yote. Anayepewa posho au kitu kingine atahitaji kuvikumbuka.

c) Mkulima anapima sehemu ya kumi yá mavuno yote. Si sehemu kumi ya pesa za nafaka uliyouza tu, bali sehemu kumi ya jumla. Tena, usisahau mazao ya wanyama, wanaofugwa kwako hasa kuku na mayai.

d) Toa sehemu ya pesa uliotoa kwa mbegu, dawa, vibarua na kadhalika. Malipo haya yote si faida bali ni njia ya kujipatia mapato yako.

e) Kumbuka ya kwamba yule aliye na moyo wa kukitetea kiasi cha matoleo kila wakati na kukipunguza iwezekanavyo, anahitaji kuangalia katika moyo wake kuona hali yake ya ndani ikiwa amedhoofika, au kuwa na hamu kupita ipaswayo kwa vitu vya dunia au nini.



B. Vifungu vya Kukaza -

1. Warumi 11:36

2. Yakobo 1:17

3. Matendo 14:17

4. I Wakorintho 6:19-20

5. Warumi 14:12

6. I Wakorintho 4:1-2

7. I Petro 4:10

# WEWE NI WAKILI WA NAFSI YAKO YOTE

## 1. Maisha Yako Yote Yaonyesha Imani Yako.

Desturi za Waafrika ni tofauti na wenzao kulingana na kabila, nchi na hata dini kw kuwatambua. Mtu anayeelewa na desturi ya kabila fulani atamtambua mmojawapo wa kabila lile kwa sura, alama za mwili, jinsi mtu anavyong'olewa meno, na uhusiano wake na Bwana Yesu Kristo kwa alama za maisha yake. Mtume Yakobo alieleza ukweli huu alipoandika katika Yakobo 2:18, "Lakini mtu atasema, wewe unayo imani, nami ninayo matendo. Nionyeshe imani yako pasipo matendo, nami nitakuonyesha imani yangu kwa njia ya matendo yangu."

Maana yake kwako kama Mkristo ni kuwa huwezi kutenganisha Ukristo wako na matendo yako yo yote. Ukiwa kazini, nyumbani, shambani, barabarani, kila tendo unalolitenda, na kila neno unalolisema, hushuhudia Ukristo wako. Watu wengine wakikuona wanajifunza juu ya Ukristo wako. Ukiwa mpole siku ya Jumapili tu, wanajua. Ukiwa mnyenyekevu kwa wakuu, na mkali kwa watumishi, mke au watoto, ni wazi mbele yao.

Kumbuka maisha haya ni uwakili, nawe unatumia ushuhuda wa matendo yako kwa busara au ovyo tu? Hutaki kuwa mtumishi asiyefaa wa Bwana wako, Mwenyezi Mungu. Na njia hii ni njia moja ya maana sana kuonyesha bidii ya uwakili wako.



b) Wengine wanasema Yesu hakupinga desturi hii bali alifuata mwenyewe. Kwa hivyo ni afadhali tuifuate pia kama desturi isiyo mbaya.

c) Wengine wanasema ya kwamba zaka ni ya Agano la Kale na Uyahudi. Haina uhusiano na Wakristo kwa hivyo mtu atoe kama anavyopenda bila kujali sehemu ya kumi. Ukitoa zaidi au chache kuliko zaka ni shauri lako tu.

d) Wengine wanaoelewa zaidi wanasema, kwa sheria si la lazima, bali kwa hali yetu, Wakristo, kama mawakili wa Mungu hatuwezi kutoa chache kuliko Myahudi. Kwa vile Kristo alitufia msalabani, kwa upendo twatoa sehemu ya kumi au zaidi. Kwa sababu ya uwakili wetu wa kuhubiri Injili kwa wote wa dunia hii, inatulazimu kutoa kwa ukarimu. Pia, kwa sababu Mungu ametubariki, tunajitoa kwake pamoja na mapato yetu. Si nzito kwetu kutoa. <u>Msingi wa Kutoa Zaka ni Moyo si Sheria</u>.

Mtu akipenda kutokutoa, anaweza kufanana na yule Kijana tajiri katika Marko 10:22, Yesu aliposema juu yake, "akaenda zake kwa huzuni; kwa sababu alikuwa na mali nyingi." Aliweka hali yake, mahitaji yake, mapenzi yake, mali yake kwanza na Mungu baadaye. Lakini wewe "Utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa." (Mathayo 6:33)

nifu kati ya Wayahudi walitoa yote ya sheria zao mpaka robo hii.

2. Zaka Katika Agano Jipya.

Sehemu ya kumi na zake zinatajwa mara nne tu katika Agano Jipya. Mara moja ni katika Waebrania 7:4-9 juu ya Agano la Kale, na mara tatu na Yesu, katika Mathayo 23:23, Luka 11:42 na Luka 18:12. Mara hizi tatu ni kwa maelezo juu ya Mafarisayo na jinsi wanavyotoa zaka na kusahau mambo mengine. Hasa maelezo inakaza desturi ya Kiyahudi. Kuna neno moja la maelezo, Yesu aliposema katika Mathayo 23:23 "Hayo (adili, rehema, imani) imewapasa kuyafanya, wala yale mengine msiyaache." Hakukataa ubora wa kutoa zaka.

Tukielewa habari za Yesu, Petro, Paulo na wengine, bila shaka walishika desturi za Kiyahudi na moja ya desturi zile ilikuwa matoleo yale ya zaka.

3. Njia Nne Za Kuamua Juu Ya Zaka.

Kwa sababu hakuna sheria kabisa katika Agano Jipya kwa Wakristo na kwa sababu Wakristo hawafuati kwa ukamilifu kila hatua katika masharti ya Kiyahudi, wewe wasema nini juu ya jambo hili?

a) Wengine wanasema Mkristo bado anafuata Agano la Kale na sheria inasema "Toa" kwa hivyo, Mkristo analazimika. Pia kufuatana na Malaki 3:8-10 mtu asipotoa fungu la kumi au zaka kamili anamwibia Mungu sehemu ya haki yake.



Pamoja na hayo, matendo, maneno, na mawazo yasiyojulikana na mtu mwingine ye yote yanajulikana na wawili, Wewe na Mungu. Utahitaji kujibu juu ya mambo haya katika siku ile ya kufika mbele ya Mungu. Je! Wataka uwakili wa matendo yako yote kuleta huzuni na hukumu ama furaha na sifa? Ni lazima shauri liwe kati ya njia hizi mbili.

2. Wakati Wako Ni Kutoka Mungu.

Tumeshataja jinsi uhai wako unavyomtegemea Mungu. Uhai huu umegawanyika katika miaka, miezi, siku, na saa. Kila miaka ambayo unayo ni kwa mapenzi ya Mungu. Kila siku unayopata ni kwa ruhusa ya Mwumbaji wako. Kila saa unayoweza uitumie kwa shughuli yo yote umepewa naye Mungu.

Hasa, Mungu katika mpango wake wa kuumba dunia hii, ameamuru ya kwamba siku moja katika saba ni takatifu na kwa matumizi yake. Katika kitabu cha Kutoka 20:8, twasoma, "Ikumbuke siku ya sabato uitakase." Ili usidhani kwamba neno hili ni kwa Waisraeli tu, ona katika Luka 4:16, ambapo Yesu "Akaenda Nazareti, hapo alipolelewa; na siku ya sabato akaingia katika sinagogi kama ilivyokuwa desturi yake." Vile vile wanafunzi wa Yesu mwenyewe, wakifuata maelezo yake waliendelea kuabudu siku moja katika juma kama siku maalum Kitabu cha I Wakorintho 16:2, chasema Wakristo waliambiwa, "Siku ya kwanza ya juma kila mtu kwenu na aweke akiba kwake, kwa kadiri ya kufanikiwa kwake." Na pia, katika Matendo 20:7, imeandikwa, "Hata siku ya kwanza ya juma, tulipokuwa tumekutana ili kumega mkate."

Kwa hivyo una uwakili wa matumizi ya siku ile katika maisha yako. Huwezi kuacha mambo ya Mungu na kusudi lake na kutumia siku ile kama upendavyo, kulima, kuvuna, kuuza na kununua katika biashara, kama siku zile sita nyingine. Mkristo anayesahau jambo hili, ameacha uwakili wa siku ambazo amepewa na Mungu na kudharau mapenzi ya Bwana wake.

Lakini, siku zinazobaki, mtu hutumia kama apendavyo? La! Hasha! Katika Yohana 9:4, imeandikwa, "Imetupasa kuzifanya kazi zake yeye aliyenipeleka maadamu ni mchana; usiku waja asipoweza mtu kufanya kazi." Kama vile una uwakili juu ya kila tendo na ushuhuda wa matumizi ya siku na kila saa.

Mkristo anajua saa zake zatoka wapi naye atapenda kuzitumia kufanya mapenzi ya yule aliyempa saa zile. Siku na saa ambapo Mkristo hukaa bure bila kusudi lo lote au bila kutumia wakati wake kwa busara, ni hasara ya kipawa cha Mungu. Zaidi, Mkristo anayetumia wakati wake kwa mambo yasiyofaa au njia zisizofaa ameharibu kipawa cha Mungu kinachopewa kwa hali ya uwakili. Je! utajibu kwa njia gani siku ile ya kuonana na Mungu uso kwa uso, akiuliza juu ya matumizi yako ya wakati aliokupatia? Utasikia huzuni na hukumu ama furaha na sifa? Ni lazima shauri liwe kati ya njia hizi mbili.

### 3. Uwezo Wako Ni Kutoka Mungu?

Msingi wa uwezo wetu wote unatoka kwa Mungu kama kipawa chake. Bila shaka umeona jinsi mtu fulani amepewa uwezo katika kuimba, kuhubiri, au kufundisha





## WEWE NA SEHEMU YA KUMI

Mwandishi mmoja, Robert Hastings, ameeleza vizuri mafunzo juu ya Mkristo na sehemu ya kumi kama matoleo yake. Alisema msingi wa kutoa kwa njia yo yote ni katika Luka 12:48, yaani "Na kila aliyepewa vingi, kwake huyo vitatakwa vingi; naye waliyemwekea amana vitu vingi, kwake huyo watataka na zaidi." Kwa sababu Wakristo wamepewa wokovu wao na baraka ya ufahamu wao wa Mwenyezi Mungu, wanastahili kutoa kwa ukarimu na upendo. Lakini, je! Kiasi gani? Sehemu ya Kumi? Kwanza tuone <u>sehemu ya kumi</u> katika Biblia. Neno <u>Zaka</u> ina maana ile ile pia katika Biblia, sehemu ya kumi inayotolewa kwa Mungu.

### 1. Zaka Katika Agano La Kale.

Neno hili linatajwa kwanza kama matoleo kwa ajili ya Mungu katika Mwanzo 14:18-20 na hapa twaona ni kutoka Ibrahimu kwa sababu ya msaada wake Mungu katika vita. Pia, Yakobo alitoa Zaka kwa Mungu katika Mwanzo 28:22. Chini ya uongozi wa Musa, Zaka ilikuwa sehemu ya sheria za Wayahudi. Soma Hesabu 18:26 na Mambo ya Walawi 27:30-32. Tumeshataja kifungu cha mwisho wa Agano la Kale, yaani, Malaki 3:8-12.

Waalimu wa Agano la Kale wanasema kuwa Wayahudi waaminifu walitozwa Zaka mara mbili kila mwaka na mara moja kila mwaka wa tatu. Kwa jumla matoleo haya yanakaribia robo ya mapokeo, lakini wami-

Neno kuu katika sababu za kutoa ni kueneza Injili. Watu huhitaji kumjua Yesu. Wengi hawajasikia, wengi ambao wamesikia hawajaamini. Msaada wa kuwapatia nafasi hii kuu ni kutoka matoleo yetu, kama tunavyosoma katika Warumi 10:13-15, "Kila atakayeliitia Jina la Bwana ataokoka. Basi wamwiteje yeye wasiyemwamini? Tena wamwaminije yeye wasiyemsikia? Tena wamsikieje pasipo mhubiri? Tena wahubirije, wasipopelekwa?"

Usipoweza kuhubiri Injili kwa wale walio mbali mwenyewe, waweza kushirikiana na msaada kwa matoleo yako.

A. Mambo Ya Kuzungumzwa -

1. Unaleta matoleo yako kwa Kanisa kwa sababu gani?

2. Kuna njia gani za kutoa kwa Mungu zisizostahili Mkristo?

3. Pesa inayowekwa katika kanisa lako inatumiwa kwa kazi gani?

B. Vifungu Vya Kukaza -

1. I Timotheo 5:8
2. Luka 16:11
3. 2 Wakorintho 8:5 na 8
4. 2 Wakorintho 9:7
5. Marko 12:41-44
6. Mathayo 6:1-4
7. Matendo 11:29
8. I Wakorintho 16:2
9. Mathayo 23:23
10. 2 Wakorintho 8:14b
11. Warumi 10:13-15



Biblia. Na kwa upande mwingine watu wengine wanaonekana kama wenye nguvu au uwezo katika ufundi fulani, biashara, ulimaji, na kadhalika. Tena wengine wanaonekana kama wapishi wema zaidi, wakarimu, wenye kuongea vizuri, au wapole.

Twahitaji kutambua ya kuwa vipawa hivi vya uwezo vinatoka kwa Mungu pia. Kila kipawa cha mtu chaweza kufahamika katika maneno ya I Wakorintho 12:4-6, "Basi pana tofauti za karama; bali Roho ni yeye yule. Tena pana tofauti za huduma, na Bwana ni yeye yule. Kisha pana tofauti za kutenda kazi, bali Mungu ni yeye yule azitendaye kazi zote katika wote."

Je! Mungu amekupa vipawa au karama gani katika maisha yako? Usipotumia ulivyopewa unafanya kinyume cha kusudi lake. Usipotumia hazitaweza kupotea? Usipotumia waweza kuhesabika kama wakili mwema wa Mwenyezi Mungu? Utasikia huzuni na hukumu ama furaha na sifa? Ni lazima shauri liwe kati ya njia hizi mbili.

4. Una Wajibu Wa Kuieneza Injili.

Yesu aliposema katika Marko 16:15, "Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe," alikuwa anawaeleza nani kazi yao? Aliposema katika Matendo 1:8 "Nanyi mtakuwa mashahidi wangu...hata mwisho wa nchi," alikuwa anawapa nani kazi yao? Wengine wamejaribu kusema ilikuwa mitume wale wa siku zile, wengine husema ni wamisheni au wachungaji lakini uwakili wa kila Mkristo unakaza ya kwamba ni wewe na washiriki wenzako na kila mtu ambaye ameupokea wokovu wa Bwana.

Hakuna ye yote ambaye amepewa wokovu wake na Mungu awezaye kusema "Si mimi." Usiseme, "Siwezi," "Sina elimu," au "Ni kazi ya mwingine." Pengine kila mtu hawezi kuhubiri au kufundisha lakini kila mtu kwa maneno na matendo ataweza kushuhudia baraka zitokazo kwa Mungu na baraka kubwa zaidi ni wokovu wetu na ushindi wetu juu ya dhambi.

Je! Utajibu kwa njia gani siku ile ya kusimama naye Mungu atakapokuuliza juu ya uwakili wako wa Injili yake? Utasikia huzuni na hukumu ama furaha na sifa? Ni lazima shauri liwe kati ya njia hizi mbili.

A. Mambo Ya Kuzungumzwa -

1. Matendo yanashuhudia uwakili wa mtu kwa njia gani?

2. Je! Mzee akiokoka anakosa kitu gani kipatikanacho na kijana anayeokoka?

3. Kuna vipawa gani vinavyoweza kutumiwa na kazi ya Mungu?

4. Kuna njia gani mtu asiye na uwezo mkubwa ataweza kushuhudia Injili?

B. Vifungu Vya Kukaza -

1. Yakobo 2:18
2. Luka 4:16
3. I Wakorintho 16:2
4. Matendo 20:7
5. Yohana 9:4
6. I Wakorintho 12:4-6
7. Marko 16:15
8. Matendo 1:8.



mnanaa na bizari na jira, lakini mmeacha mambo makuu ya sheria, yaani adili, na rehema, na imani; hayo imewapasa kuyafanya, wala yale mengine msiyaache."

3. Matokeo Ya Matoleo Ya Mkristo.

Ingawa Mkristo hatatoa kwa nia ya biashara au ya faida ya kuongezeka katika mali yake, akiamini Mungu atamwongezea matoleo yake, hawezi kukataa ya kwamba anayetoa kwa njia iliyo sawa atabarikiwa na Mungu. Pengine baraka hizi zitatoka kwa njia tofauti au za ajabu, lakini kifungu kinachojulikana zaidi kuhakikisha baraka hizi zitapewa ni Malaki 3:10, "Leteni zaka kamili ghalani, ili kiwemo chakula katika nyumba yangu, mkanijaribu kwa njia hiyo, asema Bwana wa majeshi; mjue kama sitawafungulia madirisha ya mbinguni na kuwamwagieni baraka, hata isiwepo nafasi ya kutosha, au la."

Baraka hii ni kwa anayetoa na pia hata kwa wale wanaosaidiwa na pesa zile. Hata wote wanaoshughulika na kazi ya Bwana kwa kukosa nafasi ya kufanya kazi nyingine wanaweza kusaidiwa katika riziki zao. I Wakorintho 9:14, inasema, "Na Bwana...ameamuru kwamba wale waihubirio Injili wapate riziki kwa hiyo Injili."

Pia, mara kwa mara wenye vitu vingi watasaidia wanaopungukiwa, kama ilivyoandikwa katika 2 Wakorintho 8:14, juu ya sababu ya kutoa, "Wakati huu wa sasa wingi wenu uwafae...ninyi mtakapokunguakiwa; ili mambo yawe sawasawa."

e) Kwa Kadiri Ya Baraka Na Mapokeo. Wanafunzi wa Yesu kutoka **Antiokia** waliposikia juu ya shida ya Wakristo wenzao huko Yerusalemu, Luka anatueleza katika Matendo 11:29, "Na wale wanafunzi, kila mtu kwa kadiri ya alivyofanikiwa, wakaazimu kupeleka msaada kwa ndugu zao waliokaa Uyahudi." Waliona njia ya kupima kiasi ilikuwa nini? "kwa kadiri" ya kufanikiwa. Wale waliopokea nyingi walitoa nyingi. Wale waliopokea chache walitoa chache, lakini walitoa.

f) Kwa Utaratibu. Tuliposoma katika I Wakorintho 16:2 ya kuwa,"Siku ya kwanza ya juma kila mtu kwenu na aweke akiba kwake, kwa kadiri ya kufanikiwa kwake." "Kila mtu kila juma" inaonyesha mpango hasa. Kabla Mkristo hajafika kwa ibada, apime kwa kadiri ya baraka zake na mapokeo ya juma lile akalete matoleo yake mbele ya Mungu. Ikiwa amepokea mengi, na alete kiasi cha mengi. Ikiwa amepokea machache, na alete kiasi cha machache yale. Lakini kumbuka, si kwa lazima wala huzuni, bali kwa upendo, ukarimu na upole.

Mwishowe kuna maelezo juu ya kutoa, kwa vile wachache wanapenda kusifiwa na kuonekana na wenzao. Kwa sababu hawawezi kutoa kwa furaha na ukarimu, wanajidai kutoa kuliko jinsi wanavyofanya kwa kweli. Katika Matendo 5:1-11 unakumbushwa juu ya Anania na Safira na jinsi walivyopokea ghadhabu ya Mwenyezi Mungu kwa udanganyifu wao mbele ya washiriki wengine. Na pia katika Mathayo 23:23, Yesu aliwaonya Mafarisayo wasidhani ya kuwa pesa pasipo matendo au maisha mema itatosha. Alisema, "Ole wenu...kwa kuwa mnalipa zaka za





# WEWE NI MTOAJI MBELE ZA MUNGU

## 1. Mkristo Hutoa Kwa Sababu Gani?

Jambo **muhimu** kufahamu ni kuwa kutoa mali yako kunahusika kabisa na roho yako ya Kikristo. Bila shaka kama kwa matendo mengine kutoa kunahakikisha IMANI YAKO. Katika I Timotheo 5:8, imeandikwa, "Lakini mtu ye yote asiyewatunza walio wake, yaani, wale wa nyumbani mwake hasa, ameikani Imani, tena ni mbaya kuliko mtu asiyeamini." Matoleo yetu hutumika kwa watu wetu wa jamaa ya Kikristo kwa njia zitakazotajwa baadaye. Tusipowatunza wenzetu, ndugu na dada katika Kristo, imani yetu inaonekana kuwa ndogo tu.

Vile vile kwa Mkristo kutoa katika uwakili wake kunaonyesha MAISHA YAKE YA KIROHO. Kwa vile maandiko yasema, katika Luka 16:11, "Basi, kama ninyi hamkuwa waaminifu katika mali ya udhalimu, ni nani atakayewapa amana mali ya kweli?" Maelezo yangekaza ya kwamba mali ya dunia hii haidumu kama utajiri wa kiroho. Yule Mkristo anayeendelea kujenga furaha na matumaini yake juu ya mali kuliko juu ya uwezo na msaada wa Roho wa Mungu hataweza kutegemewa kama mwenye amana ya mambo makuu ya Bwana.

Kutoa kwa Mkristo kumejengwa kwa UPENDO WA KIKRISTO. Mtume Paulo katikati ya Wakristo wa Korintho alisifu ukarimu wa Wamakedonia akisema juu yao, "Walitenda hivi si kama tulivyotumaini tu, bali kwanza walijitoa nafsi zao kwa Bwana." Na pia alisema "Sineni ili kuwaamuru,

bali kwa bidii ya watu wengine nijaribu unyofu wa upendo wenu." (2 Wakorintho 8:5 na 8). Angalia jinsi anavyounganisha kutoa na alama ya upendo wao. Twaweza kuchukua fundisho hili hapa, ya kwamba mwenye upendo mkuu atatoa alivyo navyo kwa ukarimu kuonyesha upendo ule. Kinyume cha hii ni kwamba, asiye na upendo mkuu hatakuwa tayari kutoa akiwa na nyingi au chache. Kweli kutoa kunapima kiasi cha upendo wako kwa Mungu.

2. Mkristo Hutoa Kwa Njia Gani?

Maelezo haya yanahusika na hali ya mtu na kutoa kwake kuliko mipango inayoweza kutumiwa katika makanisa yetu. Yale yataelezwa baadaye.

Ukifikiri juu ya maneno yafuatayo, bila shaka utaelewa jinsi inavyokupasa kuwaza juu ya kutoa kwako. Kifungu kizuri cha kutumia ni II Wakorintho 9:7, kinachosema, "Kila mtu na atende kama alivyokusudia moyoni mwake, si kwa huzuni, wala si kwa lazima; maana Mungu humpenda yeye atoaye kwa moyo wa ukunjufu." Maneno yanayofaa hapa ni:

a) Kwa Hiari. Kwa vile tulisoma, "kama alivyokusudia moyoni mwake;" na tena "wala si kwa lazima," Mkristo hatoi kwa sababu ya kushurutishwa, kwa kipimo fulani, kwa wakati fulani, wala kwa njia fulani. Mipango inafaa sana kusaidia watu katika kukumbuka, kupima, na kupenda kutoa, lakini mipango isifanywe hata kidogo kumlazimisha Mkristo kutoa.



b) Kwa Furaha. Tulisoma "si kwa huzuni," ni "kwa moyo wa ukunjufu." Ikiwa Mkristo hana moyo wa furaha bali anafikiria hasara yake ya pesa zile au shida zake zilizoweza kupunguka akibaki na mali ile, asitoe kwa kuwa inamlazimu atoaye kutoa kwa kupenda na kupenda kunaleta furaha.

c) Kwa Ukarimu. Hadithi ya Yesu juu ya mjane yule maskini alipofika hekaluni inaonyesha roho inayotakikana katika Mkristo akitoa mbele za Mungu. Hadithi hii iko katika Marko 12:41-44, na kiini chake kinasema, "akatia senti mbili... ametia zaidi kuliko wote wanaotia...ametia vyote alivyokuwa navyo, ndiyo riziki yake yote." Alipofikiri juu ya baraka za Mungu na ulinzi wake hakujizuia yote aliyokuwa nayo yasiwekwe katika sanduku la sadaka.

d) Kwa Upole. Mara nyingi mtu atapenda kutoa kwa kuonekana au kufahamika. Ingawa si vibaya kujua mtu gani ana ukarimu, akitamani sifa ya matoleo yake mbele ya watu,amechukua baraka yake kutoka kwa watu. Tusome sehemu ya Mathayo 6:1-4, "Angalieni msifanye wema wenu machoni pa watu, kusudi mtazamwe na wao; kwa maana mkifanya kama hayo, hampati thawabu kwa Baba yenu aliye mbinguni." Biblia haisemi mtu asionekane bali asionekane kwa kusudi la kutazamwa na kusifiwa na watu. Mara nyingi ukarimu wa mtu utachochea karama ile katika wengine. Mara nyingi italeta sifa kwa Bwana wake pia. Lakini anayetoa kwa ukarimu ajihadhari katika makusudi.